**LEARNING BY EAR 2012**

**“Wasaliti walo karibu – Hadithi inayoangazia dhulma zinazoambatana na ngono”**

**EPISODE 7: “Ni wakati wa kuamua”**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**
**EDITOR: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of Characters by scene:**

**SCENE ONE: NURU WITH DULU AT HOME**

- **Nuru (f, 30)**
- **Dulu (m, 40)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE TWO: MRS. RIMBA WITH ALLAN IN HER OFFICE**

- **Mrs. Rimba (f, 45)**
- **Allan (m, 10)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE THREE: PATO AND JUDY AT THE SCHOOL GATE**

- **Judy (f, 16)**

- **Pato (f,16)**
- **Maneno (m,45)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

## SCENE FOUR: UNCLE JOE AT THE POLICE STATION

- **Joe (m, 45)**
- **Officer (m, 45)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

## UTANGULIZI:

Hujambo na karibu katika kipindi hiki cha redio, **Noa bongo, Jenga maisha** yako. Hadithi yetu inaitwa **"Wasaliti walo karibu",** na inaangazia masaibu ya dhuluma za kingono barani Afrika. Kipindi kilichopita, Precious, mamake Allan, aliitwa shuleni na mwalimu wa mtoto wake, Bi. Rimba, aliyeshuku kuwa Allan ana jambo linalomdhili huko nyumbani. Mkutano wao ulitibuka pale Precious alipokataa katakata kuwa mwanae anadhulumiwa kingono na mpenziwe Joe, na akaondoka shuleni akiwa ameudhika mno. Kwengineko, Judy alitembelea shule ya kina Pato na kuwafahamisha kuhusu dhulma za kingono, na jinsi ya kujiepusha na kutafuta msaada. Na walipokuwa tayari wanataka kuondoa gari lao, Pato aliwakimbilia, akilia na kumuomba Judy asiondoke kabla ya kumsikiliza. Mbarika ipi itakayolipuka? Endelea kutega sikio, katika kipindi chetu cha leo kiitwacho **"Ni wakati wa kuamua".** Tunaanza na Nuru, ambae ni kafanyiwa ubakaji wa kinyama na ana majuma machache tu tangu atoke hospitali, lakini mambo sio shwari tena upande wa mume wake, Dulu.

## SCENE ONE: NURU NA DULU NYUMBANI

1. **SFX: VILLAGE ATMO. BAGS BEING ZIPPED AND PACKED**

2. **NURU:** Dulu, tafadhali – tafadhali usiondoke! Sina mwengine wakunielewa ila wewe. Askari polisi pia hawana msaada wa kunipa; daima wananidhihaki. Marafiki zangu wote wamenitenga. Wanadai nina mkosi. Hata Jena hataki tena kuzungumza nami! Kama wewe pia utaniondokea, sitakuwa na haja tena ya kuishi.

3. **DULU:** Nuru, samahani, lakini hata ukitaka kujiua mimi hilo halitaniweka. Mimi kuishi na wewe sahau. Ni ngumu kubakia kama mumewako baada ya hayo yaliotoka. Akili yangu imeshiba. Siwezi tena.

4. **NURU:** **(crying)** Lakini Dulu... Pekee yangu sitaweza. Uliona jinsi walivyonitendea! Unajua kweli ilivyo ngumu mimi kuishi katika hali hii? Wakati wote ninahofia! Hutetemeka kila wakati nionapo makundi ya wanaume . Wewe peke yako ndiye unayenielewa. Kwa sababu uliniokoa. Ningelikuwa mfu pale kisimani laiti sio msaada wako. Dulu - mumewangu – tafadhali usiniadimikie!

5. **DULU:** Sikiliza, Nuru. Sitaki kuwa mkatili kwako. Lakini hakuna anayetaka kushirikiana na wewe, yaliyotokea ni mazito… hata nami nimetengwa kwa sababu wanajua mimi ni mume wako, ikiwa kutengana na wewe ndio bei ya maisha yangu ya kawaida… niko tayari kununua uhuru wangu! Tuachane!

6. **NURU:** **(bitterly)** Unawezaje?! Eh haidhuru! Mumewangu, una uhuru wakuondoka ukitaka kutafuta maisha yako, lakini ilikuwa ni kwa ajili ya familia yangu ndipo haya yakanipata… ingelikuwa sio maji tunayotumia wote kunipeleka kisimani, nisingelifikwa na haya! Afadhali wewe unaweza kuyapata maisha yako… yangu siwezi kuyarudia

hata nikitaka!

**7. SFX: BAGS BEING DRAGGED ON FLOOR RAPIDLY**

**8. NURU:** **(weeping)** Nenda ukatafute maisha yako ya kitambo, Dulu!

**9. DULU:** Nuru… unahitaji msaada. Kuna bibi mmoja anaitwa Judy. Yeye ana shirika linalotetea waathiriwa wa dhuluma za kingono.

**10. SFX: DOOR BANGED WITH ANGER**

**11. NURU:** **(crying, inside the hut)** Tafadhali nenda, Dulu… nenda na usirudi tena!

**12. MSIMULIZI:** Upweke, lawama, hukupa uchungu zaidi hasa unapokumbwa na udhalimu kama wa kubakwa. Lakini ni masikitiko makubwa kwamba waathiriwa wa ubakaji barani Afrika hutengwa, huachwa na kubaguliwa. Uponyaji wao huchukuwa muda mrefu. Nuru ametengwa na watu waliokuwa wakimpenda na kumthamini. Anapanga kufanya nini? Usibanduke kujua kitakachotokea. Kwa sasa, Bi. Rimba bado ana wasiwasi kuhusu Allan alivyobadilika tabia zake, alimuita tena ofisini mwake.

**SCENE TWO: MRS. RIMBA WITH ALLAN IN HER OFFICE**

**13. RIMBA:** Habari, Allan. Habari ya asubuhi?

**14. Silence**

**15. RIMBA:** Allan, nakuhofia. Kwani kunaendelea nini, nikujuavyo lazima kuna jambo. Nataka ujuwe kuwa nakujali, na nataka kukusaidia, ukitaka. Nataka uwe kama vile ulivyokuwa kitambo. Allan… kuna kitu unataka kuniambia? Sitamwambia mtu yeyote. Halafu na mimi nitakusaidia.

**16. ALLAN:** **(scared)** Na je Uncle Joe? Je, akijua?

**17. RIMBA:** Allan… kwani ana nini? Kwani Uncle Joe, huwa anakuumiza? Niambie nikusaidie…

**18. ALLAN:** Mwalimu Rimba, sitaki kwenda nyumbani. Sitaki kuwa karibu na Uncle Joe tena.

**19. MSIMULIZI:** Hatua baada ya nyingine Allan alimweleza Bi. Rimba jinsi alivyokuwa akidhulumiwa na Uncle Joe, kwa kufanyiwa matendo maovu na yasiyo halali, akamweleza jinsi pia Uncle Joe alivyomuonya asithubutu kueleza mtu. Baada ya mazungumzo marefu, Rimba akaamua kuchukuwa hatua. Anajuwa Allan alihitaji msaada ili kurudia hali yake ya kawaida. Lakini kwa sasa, alijua ni vyema kumtoa kwenye shida ile, ili awe salama kwanza. Alimpeleka kituo cha polisi, na askari hawakuchukuwa muda kumkamata Uncle Joe. Sasa kutatokea nini tena? Kabla hatujagundua, tumrudie Pato. Tulimuacha mbele ya gari la Judy, baada ya Judy kuwazungumzia wanafunzi katika shule ya Pato kuhusu kusimama kidete dhidi ya dhuluma za kingono.

**SCENE THREE: PATO AND JUDY AT THE SCHOOL GATE**

**20. SFX: INSIDE THE CAR: SOUND OF CAR STARTING TO DRIVE OFF. SOMEONE KNOCKS FRANTICALLY ON THE WINDOW FROM OUTSIDE**

**21. JUDY:** **(shouts at driver)** Simamisha gari! Simama!

**22. SFX: CAR ENGINE TURNED OFF**

**23. JUDY:** Asante. Nisubirini. Nataka kumpa masikio huyu msichana nijuwe anataka kunieleza nini.

**24. SFX: CAR DOOR OPENS AND CLOSES. OUTSIDE ATMO**

**25. PATO:** **(still crying)** Siwezi tena kukubali… nimechoka… mimi ni muovu…najichukia kwa yale yaliotokea.

**26. JUDY:** Ni sawa, Bi. mdogo. Lolote lile liwalo, tunaweza kulizungumza – kwa hakika tutapata suluhisho. Unaitwa nani?

**27. PATO:** **(trying to control herself)** Pato… naitwa Pato.

**28. JUDY:** Sawa, Pato, hebu tulia… unataka kuniongelesha hapa? Au turudi tukazungumzie shule?

**29. PATO:** **(afraid)** La! hatuwezi kurudi shule. *Yuko pale*! Sitaki tena kumuona – sitaki tena kurudia niliyoyafanya. Yote uliyoyazungumza – ndiyo yamekuwa yakinitokea. Mamangu hajui. Anafurahia ati ninafuzu darasani, lakini hajui alama hizo nzuri zinatokana na nini. Kila anishikapo huhisi kutapika.

**30. JUDY:** Pato, ni sawa. Vuta pumzi kwanza, pumzika halafu uanze kunieleza tena. Nataka kujua nitakusaidiaje. Kama unaogopa na hutaki tena kurudi shule. Basi ingia kwenye gari langu. Twende kwenye shirika letu, halafu sisi wawili tu tutakuwa chumba maalumu unieleze yote yaliyokuwa yakitokea. Usijali. Msaada wote uko hapo hata kama utahitaji matibabu, madaktari wako.

**31. MSIMULIZI:** Pato alihisi uponyaji. Sasa amepata mtu wa kusema naye shida zake. Lakini kabla ya kuingia garini… Bw. Maneno anatokea ubavuni mwake...

**32. MANENO:** **(angry)** Pato! Unataka kwenda wapi?

**33. JUDY:** Ah, samahani, Mwalimu Maneno makosa ni yangu – ni mimi nimemueka hapa lakini nafikiri Pato ni …

**34. PATO:** **(very scared)** La!- hapana, Bw. Maneno…nilitaka kumuuliza kitu kabla aondoke.

**35. MANENO:** Na hicho kitu hakingelisubiri? Au hungeliweza kuniuliza mimi? Hukusikia kengele ikilia?

**36. JUDY:** Mwalimu, nimekuomba sama…

**37. MANENO:** Bi. Judy, tafadhali niache nifanye kazi yangu! Nilikuruhusu uje shuleni na kukupa muda wa kuongea, na sasa unataka kuondoka na wanafunzi bila ruhusa? Unajua hilo ni kosa kisheria?

**38. JUDY:** **(calmly)** Bw. Maneno, sikunuia kutorosha wanafunzi wako. Pato alitufuata na bila shaka ana sababu.

**39. MANENO:** **(shouts)** Pato! Rudi darasani. Haraka! Na baada ya masomo, nakutaka ofisini kwangu! Sawa?

**40. PATO:** **(afraid)** Ndio, Mwalimu Maneno.

**41. MANENO:** Bi. Judy, hebu ondoka kwenye maeneo ya shule kabla sijakuchukulia hatua. Na uelewe kuwa hii ndiyo safari ya mwisho wewe kuja hapa shule.

**42. JUDY:** **(apologetic)** Pole sana, Bw. Maneno. Tafadhali usimuadhibu Pato. Anahitaji msaada. Na nafikiri…

**43. MANENO:** Kwaheri..!

**44. SFX: FOOTSTEPS LEAVE**

**45. MSIMULIZI:** Mambo sio wakati wote huwa shwari. Pato amerudishwa darasani, na ameamrishwa na Bw. Maneno amuone ofisini. Bila shaka, Maneno amefaulu kumzuia Pato asimueleze Judy kwamba yeye ni muhusika. .. Huu ujanja wake utamfikisha wapi? Judy anaingia garini na wanaondoka. Lakini hawakufika mbali wakati Judy alipogunduwa ukweli.

**46. SFX: CAR BEING DRIVEN**

**47. JUDY:** **(instantly)** Mungu wangu! Ninafanya nini mimi? Geuza gari haraka! Tunahitaji kurudi shule haraka. Yule msichana tuliyekuwa tunazungumza naye pale shule anadhulumiwa na naibu wa mwalimu mkuu! Bw. Maneno! Kwanini sikuona haya kutokana na vitendo vyake… geuza gari turudi!

**48. SFX: CAR MAKING QUICK U-TURN**

**49. JUDY:** **(nervous)** Tuombeni tufike haraka kabla Bw. Maneno hajapata nafasi ya kumjeruhi zaidi. Nitajihisi mbaya sana ikiwa hatutafika kwa wakati ufaao... **(remorsefully)** Muathiriwa wa dhuluma za kingono ameniomba usaidizi na mimi niliondoka bila kumsaidia?

**50. MSIMULIZI:** Wakati Judy akifululiza shuleni Kilindi ili kumnasua Pato kutoka kwenye meno ya Bw. Maneno, mjombake Allan, 'Uncle Joe analetwa kituo cha polisi chini ya ulinzi mkali.

**<u>SCENE FOUR: UNCLE JOE AKIWA KITUO CHA POLISI.</u>**

**51. SFX: POLICE STATION ATMO**

**52. OFISA:** Sasa, wewe ndio yule mtu anayeharibu watoto! Haki, hata hauna haya?

**53. JOE:** Ofisa, huyo mtoto anadanganya. Hata muulize mamake. Atakwambia anadanganya.

**54. OFISA:** **(orders)** Kimya! Ile kinyoriro utatoa hapa itachukuliwa kama ushahidi kwa mahakama! Nugu wewe! Joe Zumanda, tunakuandikia mashtaka ya kudhulumu na kulawiti mtoto mdogo ya kivulana. Tutaweka wewe ndani mpaka tumarize upererezi. **(to guards)** Fungia hii ndugu ndani!

**55. SFX: IRON JAIL DOOR BEING CLOSED**

**HITIMISHO:**

Wakati lango la chuma la korokoroni linapomfungia Uncle Joe, ndipo tunapofunga kipindi hiki cha saba cha hadithi hii inayomulika maafa ya dhuluma za kingono barani Afrika. Joe atapewa adhabu gani? Judy atafaulu kumnasua Pato safari hii ya sekondari hapo shuleni? Kitamtokea nini Nuru, sasa ambavyo ameachwa na mume wake kipenzi? Usipitwe na hayo kipindi kijacho. Ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au kingine tembelea wavuti wetu www.dw.de/lbe. Pia, waweza kutoa maoni yako utakapotembelea mtandao wetu wa Facebook. Hadi kipindi kifuatacho, Kwaheri.